
# Ujumbe wa Mwenyekiti

Kufanikiwa kwa azma yetu kunategemea zaidi matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) endelevu katika kuboresha utendaji kazi wa taasisi na utoaji huduma kwa umma. Wakala ya Serikali Mtandao ni moja ya juhudi za Serikali ya Tanzania katika kuhakikisha kuwa manufaa ya TEHEMA, kama yanavyojidhihirisha katika nyanja zote za maisha ya binadamu ulimwenguni kote siku hizi, yanatumiwa ipasavyo kuchangia kufanikisha dira ya taifa ya kuwa na Serikali yenye kutoa huduma bora kwa wananchi waliohamasika katika utamaduni mpya wa kuendelea kutumia TEHAMA katika nyanja mbalimbali za maisha yao.



Mwaka 2014 ni wa pili tangu Wakala ianze rasmi kujijenga na kujitayarisha kukabili jukumu hili jipya nchini. Kwa ubunifu mkubwa wa viongozi na watendaji wote kwenye taasisi hii, tumeshuhudia mafanikio makubwa katika kila nyanja za muundo wake kama inavyofafanuliwa katika ripoti hii.

Serikali imedhamiria kuhakikisha Wakala inakuwa imara na inamudu majukumu yake kwa kuijengea uwezo na kuipatia rasilimali zinazotakiwa katika utekelezaji wa Serikali Mtandao nchini. Ni jukumu la kila mhusika katika Wakala hii kuhakikisha kuwa anatimiza wajibu wake ipasavyo.

Bodi inatambua kuwa ili kusudio la uanzishwaji wa Wakala litimizwe ipasavyo, wadau wa huduma zake nao hawana budi kwenda sambamba na jitihada za utekelezaji wa Serikali Mtandao. Taasisi za Umma hazina budi nazo kujiweka tayari kupokea na kutekeleza maelekezo shirikishi yatakayotolewa na Wakala mara kwa mara. Tutoe huduma zinazolingana kwa ubora na zenye kuonesha kuwa mkabala wetu wa matumizi sahihi ya TEHAMA ni mmoja.

Vile vile Bodi inathamini msaada mkubwa unaotolewa na wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi, na inapenda kutoa shukrani za dhati kwa misaada hiyo na kuomba moyo huo uendelee kwa manufaa ya wananchi wetu. Aidha Bodi inatambua mchango mkubwa wa mawazo na ushauri unaotolewa na viongozi wa Serikali hususan Waziri wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Katibu Mkuu wake. Ushirikiano wao unasaidia sana kuhamasisha bidii zaidi kwa watendaji wa Wakala na taasisi tunazoshirikiana nazo, hivyo kufanikisha malengo ya utekelezaji wa Serikali Mtandao nchini. Kwa hatua hii tuliyofikia, nasema asanteni sana.

# Ujumbe wa Mtendaji Mkuu

Ni mwaka mwingine tena wa kutia matumaini katika utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao nchini. Wakala imeanza kuwa na misingi imara na endelevu katika utekelezaji huo nchini. Shughuli za Wakala zimejikita zaidi katika kuhakikisha kuwa kuna sera, sheria na miongozo wezeshi inayosimamia TEHAMA katika shughuli za serikali, upatikanaji wa zana na vifaa muhimu katika kujenga miundombinu ya TEHAMA na kuweka mifumo tumizi ya Serikali Mtandao inayorahisisha utoaji huduma kwa umma kwa urahisi.

Uwezeshaji wa Wakala ili iweze kutimiza majukumu yake uliendelea vizuri. Hadi mwishoni mwa mwaka 2014, wataalam weledi wa TEHAMA na shughuli zinazohusiana na uendeshaji wa Wakala walifikia 71 ikilinganishwa na mwaka 2013 ambapo walikuwa wataalam 35, idadi ambayo inaridhisha. Aidha tuliweza kupanua nafasi ya ofisi kwa kuongeza ghorofa moja zaidi kwenye jengo la Extelecoms.



Huduma zetu zililenga zaidi uwepo wa sera, sheria na miongozo inayotoa maelekezo ikiwemo utekelezaji wa Serikali Mtandao. Uboreshaji wa mtandao wa mawasiliano Serikalini na uanzishaji wa mifumo mbalimbali inayotumika kuboresha utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa umma kwa njia ya mtandao.

Madhumuni ya ripoti hii ni kutoa muhtasari wa mafanikio ambayo Wakala imeyafikia. Wakala imehakikisha kuwa Serikali yetu imepata miundombinu na mifumo imara na ya kisasa ya TEHAMA ya kutoa huduma kwa wananchi wake. Ijapokuwa kulikuwa na changamoto mbalimbali.

Mwisho, napenda kutoa shukrani za dhati kwa viongozi wote wa Serikali waliounga mkono jitihada za utekelezaji wa Serikali mtandao nchini hususan Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, wadau wetu mbalimbali na wafanyakazi wote ambao kwa pamoja wameiwezesha Wakala kufikia mafanikio haya kama yalivyoelezwa katika taarifa hii.

# Yaliyomo


Ujumbe wa Mwenyekiti ---------- 1

Ujumbe wa Mtendaji Mkuu ---------- 2

Kuhusu Wakala ---------- 4

Muundo wa Utawala ---------- 5

Bodi ya Ushauri ya Wizara ---------- 6

Utekelezaji wa Serikali Mtandao ---------- 7

Sera, Sheria na Miongozo ---------- 9

Usimamizi na Uendeshaji wa TEHAMA ---------- 12

Miundombinu ya TEHAMA ---------- 22

Mifumo Tumizi ---------- 28

Huduma Mtandao ---------- 35

Taarifa ya Fedha ---------- 47

Habari katika Picha ---------- 49

Mwelekeo wa Kimkakati na Hitimisho ---------- 52

# Kuhusu eGA

## Historia

Wakala ya Serikali Mtandao (e-Government Agency) ni Taasisi ya Serikali iliyoundwa kwa sheria ya Wakala za Serikali Na. 30, Sura ya 245 ya mwaka 1997. Wakala imeundwa kama sehemu ya utekelezaji wa uamuzi wa Baraza la Mawaziri wa mwaka 2004 kuhusu uanzishwaji wa Serikali Mtandao; na Hati ya Rais ya Mgawanyo wa Majukumu Na. 51 wa tarehe 17 Desemba mwaka 2010 ambao umeipa jukumu na mamlaka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kutayarisha Sera ya Serikali Mtandao na kuhakikisha utekelezaji wake kwa kuanzisha Wakala ya Serikali yenye jukumu na mamlaka ya kuratibu, kusimamia na kukuza jitihada za Serikali Mtandao nchini Tanzania. Wakala ilianza kazi ya kutekeleza majukumu yake tarehe 01/04/2012 na kuzinduliwa rasmi mwezi Julai 2012.

## Dira

Kuwa Taasisi inayoongoza kiubunifu, katika kuwezesha matumizi ya TEHAMA kwa ajili ya kuboresha utoaji wa huduma kwa Umma.

## Dhamira

Kujenga mazingira wezeshi kwa ajili ya uratibu, usimamiaji na uendelezaji wa matumizi ya TEHAMA ili kuboresha utoaji wa huduma za Serikali kwa Umma.

## Misingi Mikuu

### *Uadilifu*

Wakala inafuata viwango vya uendeshaji vya hali ya juu katika kila inachofanya na inatimiza ahadi zote kwa maslahi ya Taifa.

### *Ubunifu*

Tunaamini kuwa ubunifu na fikra sahihi zinawezesha Wakala kuwa taasisi kinara na mwezeshaji katika utoaji wa huduma za Serikali Mtandao kwa wadau wa Taasisi za umma.

### *Kuthamini Wateja*

Tunaamini katika uwezo wa kila mfanyakazi kuendelea kujifunza kuhusu wateja na kuwahudumia ipasavyo kulingana na mahitaji wanayotarajia kutoka Wakala ya Serikali Mtandao.

### *Ushirikiano*

Wakala inaamini kuwa kufanya kazi kwa pamoja na kwa ushirikiano na wadau muhimu kutaiwezesha kutoa huduma bora zaidi.

### *Mwenendo Bora*

Tunaamini kwa kushirikiana na wadau wengine, tunaweza kujenga mfumo bora wa utendaji unaoweza kuigwa na taasisi nyingine za umma.

# Muundo wa Utawala



## Waziri

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ana dhamana ya kuelekeza utendaji na kudhibiti uendeshaji wa Wakala. Aidha, Waziri anabainisha Sera na mipaka ya kiutendaji ya Wakala.



## Katibu Mkuu

Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ana dhamana ya kusimamia na kutoa mwelekeo wa kisera katika utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao



## Mtendaji Mkuu

Mtendaji Mkuu ana dhamana ya kusimamia shughuli za kila siku za Wakala zikiwamo usimamizi wa rasilimali, utendaji, uendelezaji na udhibiti wa Wakala. Mtendaji Mkuu anawajibika moja kwa moja kwa Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

## Menejimenti




Menejimenti ya Wakala ina Mtendaji Mkuu, Wakurugenzi wa Idara na Mameneja wa Vitengo kulingana na muundo.

# Bodi ya Ushauri ya Wizara

Bodi ya Ushauri ya Wizara inateuliwa kila baada ya kipindi cha miaka mitatu na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Bodi hiyo ina dhamana ya kumshauri Waziri kuhusu utendaji wa Wakala. Bodi ya sasa ina wajumbe sita na Mtendaji Mkuu ni Katibu wa Bodi. (Nyadhifa zao za kikazi ziko katika mabano)

**Prof. Joseph Semboja**



Mwenyekiti
(Mtendaji Mkuu
Taasisi ya Uongozi)




**Dr Jabiri K. Bakari**

Katibu
(Mtendaji Mkuu,
Wakala ya Serikali Mtandao)

**Bw. Mohammed Pawaga**

Mjumbe
(Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi
wa Rasilimali Watu,
Tume ya Mapitio ya Katiba)





**Prof. Evelyne Isaac Mbede**

Mjumbe
(Mkurugenzi wa Sayansi na Teknolojia,
Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na
Teknolojia)

**SACP Albert Nyamhanga**

Mjumbe
(Mkuu wa Kitengo cha Sera, Mipango
na Bajeti,
Jeshi la Polisi Tanzania)





**Inj. Peter Ulanga**


Mjumbe
(Mtendaji Mkuu,
Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote)

**Bw. Priscus Kiwango**

Mjumbe
(Mkurugenzi wa Teknolojia ya Habari
na Mawasiliano,
Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi
wa Umma)



# Utekelezaji wa Serikali Mtandao



# Utangulizi

Kama ilivyo kwa nchi nyingi duniani, Tanzania inatambua umuhimu wa kutumia TEHAMA katika kuboresha utendaji wa taasisi za Serikali na za Umma ili ziweze kutoa huduma bora kwa wananchi wake. Lengo kuu ni kuhakikisha matumizi ya TEHAMA yanachangia maendeleo ya taifa na ya mtu mmoja mmoja kulingana na mipango ya maendeleo ya Taifa iliyowekwa.

Hivyo, Wakala ya Serikali Mtandao, chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma imeandaa taarifa fupi kuhusu tathmini ya utekelezaji wa Serikali Mtandao hapa nchini. Taarifa hii inalenga kutoa maelezo ya msingi kuhusu utekelezaji wa Serikali Mtandao na mafanikio yaliyopatikana. Taarifa hii itaiwezesha Serikali na watendaji wake wakuu kuwa na taarifa muhimu kuhusu Serikali Mtandao na namna TEHAMA inavyoiwezesha Serikali katika kupanga na kutekeleza mipango mbalimbali ya maendeleo kitaifa kama vile: Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Tanzania (MKUKUTA), Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, 2011/12 – 2015/16 na Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa “BRN”.

# Dhana ya Serikali Mtandao

Serikali Mtandao ni matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwa lengo la kuboresha utoaji wa huduma kwa Umma, kuhamasisha ushirikishwaji wa raia katika utoaji wa uamuzi unaowahusu na kuwezesha kuwepo na Serikali iliyo wazi, inayowajibika na makini katika kutekeleza majukumu yake kwa taifa.

# Malengo ya Serikali Mtandao

Serikali Mtandao ina malengo makuu matano. Lengo la kwanza ni kuimarisha utawala bora na kuongeza tija na ufanisi katika uendeshaji wa taasisi za umma kwa kuhakikisha kuwepo kwa mawasiliano ya haraka, yenye uhakika na salama ndani na miongoni mwa taasisi mbalimbali za Serikali kuanzia kwenye Wizara, Mikoa hadi ngazi za Halmashauri pamoja na Balozi zetu nje ya nchi.

Lengo la pili ni kupunguza gharama za mawasiliano na usambazaji wa taarifa mbalimbali. Lengo la tatu ni kupanua wigo wa upatikanaji wa taarifa muhimu katika kila ngazi Serikalini, mahitaji mbalimbali ya taarifa kati ya Serikali na wananchi, wazalishaji, wawekezaji na wadau wote wa ndani na nje ya nchi.

Lengo la nne ni kuimarisha usalama wa Serikali na raia wake katika karne ya sayansi na teknolojia na kuongeza uwezo wa Serikali kupambana na majanga kwa kutumia teknolojia; na lengo la tano ni kurahisisha michakato ya utendaji kazi katika taasisi za Serikali na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.

Hivyo basi, taarifa hii inajumuisha mafanikio ya utekelezaji wa Serikali Mtandao yaliyojikita katika misingi mikuu mitano ambayo ni, Sera, Sheria na Miongozo, Usimamizi wa TEHAMA, Miundombinu ya TEHAMA, Mifumo Tumizi (Application Systems) na Huduma Mtandao (e- services).

# Sera, Sheria na Miongozo

Utekelezaji wa Serikali Mtandao unategemea kuwepo kwa Sera, Sheria, Kanuni, Miongozo na Mikakati Madhubuti ili kuboresha utoaji huduma kwa umma.

# Sera, Sheria na Miongozo

Utekelezaji wa Serikali Mtandao unategemea kuwepo kwa Sera, Sheria, Kanuni, Miongozo na Mikakati Madhubuti ili kuongoza utekelezaji sahihi na kulinda maslahi ya utekelezaji na watumiaji wa huduma zitolewazo na Serikali. Katika eneo hili Serikali imeendelea kufanya juhudi zifuatazo:

## Sera

Mchakato wa kupitia na kuboresha Sera ya Taifa ya TEHAMA ya mwaka 2003 upo katika hatua za mwisho. Sera hii inaakisi malengo ya kitaifa yaliyoainishwa kwenye Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025.


Rasimu ya Sera ya Serikali Mtandao imekamilika na itawasilishwa katika kikao cha Wadau. Sera hii ina lengo la kuifanya Serikali ya Tanzania kuongoza katika ubunifu wa utoaji huduma zinazowezeshwa na TEHAMA




## Sheria

Sheria ya "Electronic and Postal Communications" 2010. Sheria hii inasimamia maendeleo ya mawasiliano ya kimtandao kwa kuweka uratibu na udhibiti wa Sekta ya mawasiliano na huduma za posta, kuanzisha mfumo wa usajili na utoaji wa leseni katika sekta mawasiliano, kudhibiti ushindani katika sekta ya mawasiliano na kuainisha makosa na adhabu katika sekta hiyo.

Sheria ya "Electronic Transactions Act" na Sheria ya "Cybercrimes Act" zimepitishwa na Bunge 2015. Mswaada wa sheria ya "Personal Data Protection Act, 2014", upo kwenye maandalizi. Sheria hizi zinalenga kuimarisha udhibiti na kuboresha utekelezaji wa masuala yanayohusu TEHAMA nchini.



## Miongozo

Miongozo hulenga kutoa maelekezo kwa watekelezaji kufuata maelekezo na utaratibu sahihi katika matumizi ya TEHAMA Serikalini. Aidha, miongozo inatoa maelekezo na ufafanuzi wa taratibu zinazotakiwa kufuatwa katika utekelezaji wa juhudi mbalimbali zinazohusu TEHAMA katika taasisi za umma.

Ili kuhakikisha kuwa utekelezaji wa Serikali Mtandao unafanyika katika viwango vinavyotakiwa, Serikali inatengeneza muongozo na viwango vya utekelezaji wa Serikali Mtandao ambao unajumuisha viwango vinavyolenga kuhakikisha kuwa Taasisi za Umma zinatekeleza jitihada za Serikali Mtandao katika viwango na ubora unaotakiwa.



# Usimamizi na Uendeshaji wa TEHAMA

Usimamizi na Uendeshaji wa TEHAMA katika utekelezaji wa Serikali Mtandao unategemea uongozi bora wa TEHAMA, Muundo wa usimamizi wa TEHAMA Serikalini madhubuti, uratibu na udhibiti wa miradi ya TEHAMA na uendelezaji rasilimali watu inayosimamia utekelezaji huo.



*Mtendaji Mkuu wa Wakala Dkt. Jabiri Bakari akitoa ufafanuzi wa jambo kwa Waziri wa Fedha Mhe. Saada Mkuya (Mb)(kushoto) na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma Mhe. Celina Kombani (Mb) (katikati) baada ya utambulisho wa Afisa Tehama Mwandamizi aliyekuwa katika mafunzo ya kupandisha taarifa kutoka Manispaa ya Temeke Bi. Beatrice Ntyangiri wakati wali-potembelea ofisi za Wakala, Desemba 4, 2014.*

# Uongozi wa TEHAMA Serikalini

Serikali Mtandao ni moja ya agenda katika kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na mipango mingine ya maendeleo ya Taifa. Aidha, utekelezaji wa Serikali Mtandao unatambuliwa na kupewa msukumo na uongozi wa juu nchini akiwemo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wasaidizi wake.

Kiwango cha juu cha utekelezaji wa Serikali Mtandao kitafikiwa endapo vipaumbele vitatolewa katika eneo hili katika ngazi zote za uongozi. Uzoefu katika Mataifa yaliyofanikiwa katika utekelezaji wa Serikali Mtandao unaonyesha kuwa utashi wa viongozi katika ngazi mbalimbali na agenda ya Serikali Mtandao kuwa sehemu ya mipango mikuu ya nchi husika, hutoa mchango mkubwa katika mafanikio hayo.



*Menejimenti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na ya  Wakala Serikali Mtandao wakiwa katika kikao cha pamoja kilichofanyika katika ofisi za Wakala, Februari 9, 2015.*

## Mipango Mkakati

Mipango Mkakati inalenga kutoa mwelekeo wa kila taasisi katika kubuni, kutumia na kudhibiti matumizi ya TEHAMA katika kuboresha utoaji wa huduma kwa umma na kuboresha taratibu za utendaji kazi ndani ya Serikali. Mipango hii inasaidia taasisi kufikia malengo yake ya kimkakati kupitia matumizi ya TEHAMA.

Mipango Mkakati hiyo ni pamoja na Mpango Mkakati wa Serikali Mtandao wa mwaka 2012, na Mipango Mkakati ya TEHAMA katika taasisi za umma. Taasisi mbalimbali za umma zimepewa ushauri wa kitaalam katika kutengeneza Mipango Mkakati ya taasisi hizo.



*Mtendaji Mkuu wa Wakala Dkt. Jabiri Bakari akimuonyesha Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Huria (OUT), Prof. Tolly Mbwete sehemu ya Mpango Mkakati wa Wakala wakati alipotembelea Ofisi za Wakala Agosti 6, 2014. Katikati ni Mkurugenzi wa Huduma na Uwezeshaji wa Wakala SSP. Ibrahimu Mahumi.*

# Uratibu wa Miradi ya TEHAMA Serikalini

Jitihada za Serikali Mtandao zinahitaji uratibu na usimamizi wa miradi ya TEHAMA iliyoanzishwa Serikalini. Uzoefu wa nchi zilizoendelea katika eneo la TEHAMA na Serikali Mtandao unaonesha kuwa juhudi kubwa zimefanyika katika uratibu na usimamizi wa jitihada zinazoendelea katika taasisi husika.

Utaratibu uliokuwepo kabla ya Waraka wa Mkuu wa Utumishi wa Umma Na. 3 wa mwaka 2013 ulizifanya kila taasisi kuwa na mikakati mahususi ya utekelezaji kulingana na vipaumbele vyake bila kuwa na taarifa ya mipango inayoendelea kwenye maeneo mengine. Hali hii imesababisha kuwepo mipango inayofanana ya kujenga mifumo mikubwa na yenye mahitaji makubwa ya kifedha kwa taasisi za Serikali. Aidha ukosefu wa uratibu na udhibiti wa kutosha wa kimfumo uliongeza kasi ya miradi hii ambayo mingine inategemea mikopo kutoka kwa wadau wa maendeleo na mashirika ya kifedha ya kimataifa.

Kwa sasa, Wakala inafuatilia na kuzishauri taasisi mbalimbali zinazoandaa na kutekeleza miradi ya TEHAMA kwa kutumia Miongozo ya kitaalamu ili kuhakikisha mradi hiyo inatimiza malengo yaliyokusudiwa na inakua endelevu. Taasisi zaidi ya 27 zimeshauriwa katika kubuni na kuendesha miradi yake ya TEHAMA.


Miongozo inayotumika katika uratibu na usimamizi wa miradi ya TEHAMA Serikalini ni pamoja na Mwongozo wa Matumizi Bora, Sahihi na Salama ya Vifaa na Mifumo ya TEHAMA Serikalini wa mwaka 2012, Waraka wa Mkuu wa Utumishi wa Umma Na 3 wa mwaka 2013 kuhusu Utaratibu wa Utekelezaji wa Mifumo Mbalimbali ya TEHAMA katika Utumishi wa Umma. Miongozo mingine ni pamoja na Orodha hakiki, Vigezo na hatua zinazotumika kuthibitisha miradi ya TEHAMA Serikalini.

Ili kuhakikisha uratibu na usimamizi wa miradi ya TEHAMA Serikalini unafanyika kwa ufanisi, Wakala imetengeneza mfumo wa Usimamizi wa Miradi ya TEHAMA Serikalini unaopokea na kutunza taarifa za miradi ya TEHAMA iliyopo na inayotarajiwa kuanzaishwa Serikalini.



# Mfumo wa Usimamizi wa Miradi ya TEHAMA Serikalini

Ni mfumo unaotumika kupokea taarifa za miradi inayotarajiwa kuanzishwa kwenye taasisi za Serikali ambapo Wakala ya Serikali Mtandao itapitia na kutoa maoni yake kitaalamu. Vilevile, mfumo huu unakusanya taarifa zote za TEHAMA kwa taasisi zote za serikali kuanzia Rasilimali watu, Miongozo iliyopo, Mifumo, Miradi na Vihifadhi Mifumo (Servers). Mfumo huu utawezesha kupata taarifa sahihi za hali ya TEHAMA Serikalini kila wakati, kuwezesha uratibu wa shughuli za TEHAMA zinazoendelea Serikalini na kuwezesha Serikali kupanga na kutoa uamuzi kwenye mambo mbalimbali yanayohusiana na kufanya uamuzi.





# Mfumo wa Huduma kwa Wateja

Zipo changamoto nyingi zinazowapata wateja wanaotumia huduma za Serikali kutokana na kutawanyika kwa vyanzo mbalimbali vya kupata habari ambavyo husababisha mteja kutofahamu mahali anapoweza kuwasilisha tatizo alilonalo ama kupata huduma stahiki kwa wakati. Kwa kuzingatia hili, Wakala imebuni mfumo wa huduma kwa wateja maalum kwa kutoa huduma za msaada wa kiufundi unaotumiwa na wataalamu wa TEHAMA kwa ajili ya mawasiliano na taasisi zote za Serikali zinazotumia huduma za Wakala saa 24 siku 7 za wiki.

Mteja anaweza kuwasilisha maombi au matatizo ya kiufundi ya huduma zinazotolewa na Wakala kupitia anuani ya mfumo www.helpdesk.ega.go.tz au kutuma baruapepe egov.helpdesk@ega.go.tz.

Pia anaweza kutuma maombi au matatizo hayo kwa kutumia simu namba +255 764 292 299. Mteja atapewa nywila na jina la mtumiaji pindi atakapoingia kwenye mfumo huo, atapewa namba ya mrejeo atakayoitumia kutuma maombi hayo.




e-Government Agency
Help Desk System
DASHBOARD
CUSTOMERS
TICKETS
SERVICES
CMDB
CHANGES
CUSTOMER FEEDBACK
STATISTICS
ADMIN
Dashboard
REMINDER TICKETS
My locked tickets (0) | My responsibilities (0) | Tickets in My Queues (0) | All tickets (0)
TICKET# AGE TITLE
none
ESCALATED TICKETS
My locked tickets (15) | My responsibilities (14) | Tickets in My Queues (0) | All tickets (334)
1 2 3 4 5 >> >|
TICKET# AGE TITLE
2015021610193 2 h 50 m Problem with my Desktop
2015021610191 5 h 50 m 2015 Auction sales on used cars!...
2015021410186 2 d 0 h East Africa Public & Private Sector Management & Leadership Symposium ....Kampala Uganda
2015021510187 20 h 50 m Technical check result
2015021410182 2 d 10 h Notification about cancellation of the domain transport.go.tz
2015021510189 16 h 50 m Advanced Talent Management Training
2015021410184 2 d 0 h East Africa Public & Private Sector Management & Leadership Symposium ....Kampala Uganda
2015021310181 2 d 17 h Spam email forwarded
2015021310180 2 d 21 h INTERNET SERVICE
2015021310179 2 d 21 h INTERNET SERVICE
NEW TICKETS
My locked tickets (11) | My responsibilities (8) | Tickets in My Queues (0) | All tickets (332)
1 2 3 4 5 >> >|
TICKET# AGE TITLE
2015021610193 2 h 50 m Problem with my Desktop
2015021610194 2 h 50 m Problem with my Desktop
2015021610191 5 h 50 m 2015 Auction sales on used cars!...
2015021610192 5 h 50 m 2015 Auction sales on used cars!...
2015021510190 16 h 50 m Advanced Talent Management Training
SETTINGS
7 DAY STATS
200
100
0
Tue Wed Thu Fri Sat Sun Mon
UPCOMING EVENTS
none
HELP DESK ONLINE CUSTOMERS
paul paul(0)

# Rasilimali Watu Katika TEHAMA

Serikali ilihuisha muundo wa utumishi kwa kada ya TEHAMA ili kupata watumishi wenye viwango na ujuzi unaohitajika kulingana na ushindani uliopo katika soko la ajira na mahitaji yanayotokana na ongezeko la mahitaji ya utoaji wa huduma za Serikali kwa kutumia TEHAMA. Muundo huo mpya umeanza kutumika 2014.

Aidha ili kufanya wataalam wa TEHAMA kuwa wabunifu katika kushughulikia kazi zao za msingi Wakala imetoa mafunzo mbalimbali kwa taasisi ili kuwajengea uwezo Maafisa TEHAMA na watumishi wengine kutoka taasisi za serikali ili kuweza kurahisisha utekelezaji na jitihada za Serikali Mtandao nchini. Wakala imetoa mafunzo ya kusimamia Mtandao Unganishi wa Serikali (Govnet) na mafunzo ya 'Cyberoam' kwa taasisi 83 za Serikali ili kuweza kusaidia katika masuala ya utawala, uendeshaji na matengenezo ya mtandao Serikalini pamoja na kuziongezea ujuzi wa kumudu vifaa hivyo. Mafunzo mengine ni ya Uendeshaji wa Vituo vya Data na Usimamizi wa Mfumo wa Baruapepe Serikalini (GMS) kwa taasisi 91 mbalimbali za umma yanayolenga kuongeza uwezo wa kutoa huduma bora katika matumizi ya mfumo huo.



*Maafisa Waandamizi wa TEHAMA Serikalini kutoka Mkoa wa Morogoro wakiwa katika mafunzo ya jinsi ya kuandaa na kupandisha taarifa katika tovuti zao.*




*Maafisa Waandamizi wa TEHAMA Serikalini kutoka Mkoa wa Dar es Salaam wakiwa katika mafunzo ya jinsi ya kuandaa na kupandisha taarifa katika tovuti zao.*



*Maafisa Tehama waandamizi wa mkoa wa Dar es Salaam wakiwa katika mafunzo ya ya jinsi ya kuandaa na kupandisha taarifa katika tovuti zao yaliyofanyika katika ofisi za wakala jijini Dar es salaam, Oktoba Novemba 3-7, 2014*

# Miundombinu ya TEHAMA

Miundombinu bora na shirikishi ya TEHAMA ni muhimu katika kuboresha utoaji wa huduma kwa umma. Miundombinu iliyopo ni pamoja na Mkongo wa Taifa (NICTBB), Mtandao wa Serikali (GovNet), Vituo vya Kitaifa vya Data, Masafa ya intaneti.

# Miundombinu ya TEHAMA Serikalini

Kwa kuzingatia umuhimu wa usalama wa uhakika wa Miundombinu ya TEHAMA Serikali inaweka miundombinu ya TEHAMA ambayo itaziwezesha taasisi za umma kushirikiana katika matumizi ya rasilimali za TEHAMA ili kuondoa urudufu, kupunguza gharama na kuongeza ubora wa huduma zinazotolewa kwa umma na kuhakikisha usalama wa mawasiliano. Miundombuni hiyo ni kama ifuatavyo: Mkongo wa Taifa (NICTBB)





## Mkongo wa Taifa (NICTBB)

Mkongo huu ulianzishwa mwaka 2006 kwa lengo la kuweka msingi imara wa mawasiliano ya kielektroni nchini. Unaunganisha mikoa yote ya Tanzania, Nchi za Afrika na Kimataifa kwa kutoa mawasiliano ya haraka ya sauti na taarifa. Mkongo huu unaboresha mawasiliano kati ya taasisi za Serikali na unarahisisha huduma mtandao zinazotolewa na taasisi mbalimbali za Serikali kupatikana kwa ufanisi na kwa gharama nafuu.

Mikoa yote ya Tanzania Bara imeunganishwa katika awamu ya kwanza na ya pili na awamu ya tatu itahusisha Wilaya, Miji na Zanzibar na hivi sasa unatumiwa na kampuni za simu.

# Mtandao wa Serikali (GovNet)


Mfumo huu unaunganisha Taasisi zote za umma kwenye mtandao mmoja wa mawasiliano ambao ni salama na wenye gharama nafuu, una lengo la kuziwezesha taasisi za Serikali kuwa na mawasiliano ya kielekton (data, sauti na video) ya ndani. Hadi sasa Wizara, Idara na Wakala 72 zimeunganishwa na Taasisi 77 za Mamlaka ya Serikali za Mitaa zitaunganishwa katika mtandao huo. Taasisis 50 zinatumia huduma zinazopatikana katika mfumo huo.




*Mtendaji Mkuu wa Wakala Dkt. Jabiri Bakari akifafanua kwa Waziri wa Fedha Mhe. Saada Mkuya(Mb) na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma Mhe. Celina Kombani (Mb) jinsi miundombinu ya Tehama itakavyosimamiwa kwa kutazamwa na watalaam kwa saa 24/7 wakiwa katika kituo kimoja wakati walipotembelea ofisi za Wakala.*


# Vituo vya Kitaifa vya Data

Vituo hivi vitatumika kuhifadhi data za kielektroni kwa taasisi mbalimbali nchini, asilimia 25 zitatengwa kwa ajili ya matumizi ya Serikali Mtandao. Vituo hivi vitatumika kama vituo mbadala pale vituo vya Kitaifa vya Data vitakapoanza kutumika rasmi. Hivi sasa Wakala inahifadhi mifumo tumizi ya TEHAMA na tovuti kutoka taasisi mbalimbali za Serikali.



# Masafa ya intaneti (Internet Bandwidth)

Serikali kupitia mradi wa RCIP imenunua haki miliki za kutumia (Indefeasible Right of Use (IRU)) 1.55 Gbps kwa muda wa miaka 10 ambapo Taasisi za Serikali 160 zimeunganishwa na "bandwidth". Maeneo yaliyopewa kipaumbele ni kama vile Hospitali, Shule na Taasisi za Elimu ya Juu. Upatikanaji wa masafa haya utasaidia kuboresha utoaji wa huduma kwa jamii.



# Mikutano kwa Njia ya Video

Mikutano kwa njia ya Video (Video Conferencing) ni miundombinu inayounganisha Mikoa na Wizara zote ili kuwezesha kufanya mikutano kwa njia ya video. Mwongozo wa Matumizi ya Mawasiliano kwa Njia ya Video Serikalini wa Mwaka 2014 unaotoa maelekezo ya matumizi sahihi ya mikutano kwa njia ya video umetolewa 2014 na umesambazwa kwa taasisi zote za Serikali. Wakala inaandaa utaratibu ambao utahakikisha usalama katika ubadilishanaji wa taarifa wakati wa mikutano hiyo.



*Menejimenti ya Utumishi wa Umma ikifanya mkutano kwa njia ya video.*

# Mifumo Tumizi

Serikali imeendelea kutengeneza mifumo tumizi ya kimkakati inayorahisisha utendaji kazi wa Serikali na mifumo ya kisekta inayorahisisha utoaji wa huduma kwa umma.

# Mifumo Tumizi


Serikali inategemea mifumo ya TEHAMA ili kuboresha na kurahisisha utendaji kazi na utoaji huduma kwa umma. Mifumo hiyo imegawanyika katika maeneo makuu mawili ambayo ni Mifumo Tumizi ya Kimkakati na Mifumo ya Kisekta.

Mifumo Tumizi ya Kimkakati inajumuisha mifumo inayohusika na utambulisho wa wananchi kama vile Mfumo wa Usajili wa Vizazi na Vifo, Mfumo wa Vitambulisho vya Taifa (NIDA) na Mfumo wa Utoaji wa Hati za Kusafiria (Passport).

Mifumo mingine ya kimkakati ni Mifumo ya fedha kama vile, Mfumo wa Fedha Unatumika katika Usimamizi wa Mapato (TANCIS), Mfumo wa Usimamizi wa Fedha (IFMIS) na Mfumo wa Ununuzi Serikalini (e-Procurement).


Kundi jingine la mifumo ya kimkakati ni Mifumo ya Uendeshaji kama vile, Mfumo Shirikishi wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS), Mfumo wa Barua Pepe Serikalini (GMS) na Mfumo wa kuratibu Huduma za Ardhi (LMIS)

# Mfumo wa Fedha wa Usimamizi wa Mapato (TANCIS)



# Mfumo Shirikishi wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS)

Mfumo huu unatumika kusimamia rasilimali watu katika utumishi wa umma; kukusanya, kukokotoa, kutunza na kuwasilisha taarifa mbalimbali za Watumishi wa Umma kuhusu masuala ya kiutumishi na mishahara.



# Mfumo wa Barua pepe Serikalini

Mfumo huu unasaidia kurahisisha mawasiliano ya barua pepe kwa watumishi wa Serikali na kuongeza usalama wa taarifa zinazosafirishwa kwa mfumo huo. Mfumo huu ulianza kufanya kazi Desemba, 2014 na mpaka sasa taasisi 41 za umma zinautumia. Aidha mfumo huu umeunganishwa na Mfumo Shirikishi wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara HCMIS .

Pia mafunzo ya uendeshaji wa mfumo huu yametolewa kwa watumishi 162 kutoka taasisi 91 ambapo mchakato wa taasisi hizi kuanza kutumia mfumo huu upo kwenye hatua mbalimbali.



# Mifumo ya Kisekta

Mifumo hii inalenga kuboresha mifumo ya Serikali Mtandao kwenye maeneo mahsusi ya sekta za Elimu, Afya, Maji, Viwanda, Biashara, Nishati, Madini, Kilimo, Maliasili, Utalii, Ardhi, Fedha, Mawasiliano, Ujenzi, Uchukuzi, Mifugo, Uvuvi, Ajira, Michezo na Sheria. Wakala inatoa ushauri wa usimamizi na uendeshaji wa mifumo hiyo na inahakikisha kuwa mifumo hiyo inabadilishana taarifa na inahifadhiwa kwa usalama .



***Mtendaji Mkuu wa Wakala Dkt. Jabiri Bakari (Kulia) akimweleza Kamishina wa Bajeti Bw. John Cheyo (kushoto) jinsi Tovuti na Mifumo ya Taasisi za Serikali inavyohifadhiwa wakati alipotembelea Ofisi za Wakala, Februari 12, 2015. Katikati ni Mkurugenzi wa Udhibiti wa Huduma za Serikali Mtandao Bw. Michael Moshiro.***


# Huduma Mtandao

Serikali imetengeneza Tovuti Kuu mbalimbali zinazorahisisha utoaji wa taarifa na huduma kwa wananchi kwa haraka, uwazi, urahisi, gharama nafuu kwa wakati wowote na mahali popote nchini.

# Tovuti Kuu ya Serikali


Tovuti Kuu ya Serikali (www.tanzania.go.tz) ni dirisha moja la utoaji wa huduma na taarifa kwa umma. Maudhui ya Tovuti Kuu hiyo yanapatikana kwa lugha ya Kiingereza na Kiswahili na yamegawanyika katika sehemu kuu saba. Sehemu hizo ni pamoja na Serikali, Wananchi, Taifa Letu, Biashara, Sekta, Mambo ya Nje na Nifanyeje.

Aidha katika Tovuti Kuu kuna nakala za Sheria 1,427; fomu 640, Kanuni na taratibu 153, Gazeti la Serikali 136, Sera 94, hotuba za Viongozi wa Kitaifa 356, Nyaraka 173, Miundo ya Utumishi 25, Hotuba za Bajeti 104, Takwimu 51 na Mikataba ya Kimataifa 63 na Nifanyeje yenye huduma 101.




## Sheria

Kipengele hiki kina sheria mbalimbali zinazotumika nchini Tanzania zilizotungwa na Bunge au Baraza la Wawakilishi, sheria za Kimila na mapokeo ambapo ndani yake kuna sheria kuu na ndogo ndogo. Hadi sasa, jumla ya sheria 1,427 zimeingizwa kwenye Tovuti Kuu.




## Gazeti la Serikali

Gazeti Rasmi la Serikali huchapisha miswada, sheria zilizopitishwa kabla na baada ya ridhaa, sheria ndogo, matangazo ya uteuzi wote unaofanywa na Serikali na tarehe za kuanza kutumika kwa sheria. Gazeti hili huchapwa Mpigachapa wa Serikali na mpaka sasa jumla ya matoleo 144 yanapatikana kwenye Tovuti Kuu ya Serikali.




## Mpangilio Orodha

Kipengele hiki kinaonyesha taarifa za mawasiliano na ramani (anuani za makazi) kuhusu Wizara, Idara, Wakala za Serikali, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mahakama, Hospitali, Elimu, na Mashirika ya Kimataifa na Ofisi za Balozi zinazoweza kupatikana kwa kuchapa neno la msingi la ofisi inayotafutwa.




## Nifanyaje

Sehemu hii huwapa wananchi taarifa kuhusu taratibu na masharti ya kuzingatia wakati wa kutafuta huduma kutoka kwenye taasisi za umma. Sehemu hii ina kivinjari kitakachokuwezesha kutafuta taarifa unayotaka kwa kuchagua ofisi ya Serikali, kundi au kwa kuchapa neno la msingi la taarifa inayotafutwa. Mwananchi atapata taarifa muhimu anazozitaka kama vile kuomba pasipoti, kutoa malalamiko, kuomba Uraia, Kulipa kodi, Kupata vyeti, kununua nyumba, kupata leseni na kuomba vibali.



# Tovuti Kuu ya Ajira

Tovuti Kuu ya Ajira www.portal.ajira.go.tz, Mfumo huu upo chini ya Sekretarieti ya Ajira ambao una lengo la kurahisisha mchakato wa ajira Serikalini kwa kupunguza gharama, muda na unaongeza uwazi katika taratibu za uombaji kazi na usaili. Mfumo huu ni dirisha kuu la kutangaza nafasi za kazi Serikalini ambapo wanaotafuta kazi watapaswa kuweka taarifa zao mara moja kwenye tovuti hiyo na pindi zinapotokea nafasi za kazi watataarifiwa kupitia barua pepe au simu ya mkononi *152*00# na kuweka majina yao kwenye orodha fupi ya waajiriwa watarajiwa kulingana na mahitaji ya nafasi iliyotangazwa. Mfumo huu unafanyakazi na mpaka sasa kazi 6500 zimetangazwa kwa kutumia mfumo huo.




# Tovuti Kuu ya Takwimu Huria

www.opendata.go.tz/ ni dirisha moja la kutolea takwimu huria mbalimbali za Serikali ili kusaidia wananchi na wadau wengine kupata taarifa na takwimu za uendeshaji wa Serikali kiurahisi na kuzitumia katika jitihada za maendeleo kiuchumi na kijamii.


Sekta zilizopewa kipaumbele kwa kuainishwa katika mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN) ambazo taarifa za Takwimu zinazopatikana katika tovuti hiyo ni Elimu, Afya na Maji. Takwimu hizo zinaweza kutumika na taasisi mbalimbali za kiraia, wachumi, wanasiasa, wasomi na viongozi mbalimbali.

Tovuti Kuu ya Takwimu inasimamiwa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) ambayo ipo chini ya Wizara ya Fedha na Wakala ya Serikali Mtandao na Idara ya Uhifadhi wa Kumbukumbu na Nyaraka zilizopo chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.



# Tovuti ya Wananchi

Tovuti ya Wananchi, http://wananchi.go.tz, ipo chini ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo – Idara ya Habari Maelezo inawawezesha wananchi kuwasiliana moja kwa moja na Serikali yao, kuwasilisha kero, maoni na hoja zao mbalimbali kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali na utumishi wa umma kwa jumla. Utendaji kazi wa Tovuti hii unaimarisha na kupanua dhana ya uwazi na uwajibikaji Serikalini ili kuboresha utawala bora nchini.



# Mifumo na Tovuti za Taasisi Zilizotengenezwa na Wakala

Juhudi zinaendelea kuhamasisha uanzishwaji wa mifumo mbalimbali na tovuti zinazotoa huduma na taarifa kwenye zile taasisi za umma ambazo hadi sasa hazina. Takriban taasisi 200 tu zenye tovuti kati ya taasisi 405 za Serikali zina tovuti. Kipaumbele kimewekwa katika Halmashauri ambazo nyingi hazina Tovuti. Mpaka sasa taasisi 35 zimetengenezewa tovuti zikiwemo Halmashauri za Mkoa wa Mtwara na Mkoa wa Morogoro.

- www.tanzania.go.tz
- www.portal.ajira.go.tz
- Government Mailing System
- www.wananchi.go.tz
- www.opendata.go.tz
- www.govsms.ega.go.tz
- www.helpdesk.ega.go.tz
- www.gip.ega.go.tz
- Public Service Commission MIS

1. www.ikulu.go.tz
2. www.chiefsecretary.go.tz
3. www.opengov.go.tz
4. www.morogoromc.go.tz
5. www.muungano.go.tz
6. www.bungemaalum.go.tz
7. www.kazi.go.tz
8. www.habari.go.tz
9. www.dcc.go.tz
10. www.morodc.go.tz
11. www.mvomero.go.tz
12. www.temeke.go.tz
13. www.ega.go.tz
14. www.nec.go.tz
15. www.nanyunbu.go.tz
16. www.tandahimba.go.tz
17. www.dodoma.go.tz
18. www.ulanga.go.tz
19. www.ilala.dc.go.tz
20. www.ucsaf.go.tz
21. www.psc.go.tz
22. www.tanroads.go.tz
23. www.gairo.go.tz
24. www.kec.go.tz
25. www.kilombero.go.tz
26. blog.ikulu.go.tz
27. www.nfra.go.tz
28. www.ega.go.tz
29. www.kilosa.go.tz
30. www.mtwara.go.tz
31. www.masasitc.go.tz
32. www.masasidc.go.tz
33. www.wdmi.ac.tz
34. www.apshrmnet.go.tz
35. www.moi.ac.tz



*Mkurugenzi wa Udhibiti wa Huduma za Serikali Mtandao, Bw. Michael Moshiro akiwasilisha mada katika kikao cha wadau cha kujadili huduma za Serikali zitakazotolewa kwa njia ya simu za mkononi, kilichofanyika katika ukumbi wa Hoteli ya Giraffe (Mbezi Beach), Februari 23, 2015.*

# Huduma za Serikali kwa Kutumia Simu za Mkononi

Tanzania imeanza kutumia huduma za miamala ya fedha kwa kutumia simu za mkononi kama vile M-PESA, Tigo Pesa, "Airtel Money"na Z-PESA kuanzia mwaka 2008. Huduma hiyo imesadia kuboresha na kurahisisha utumaji, upokeaji fedha kutoka sehemu moja kwenda nyingine hasa maeneo ya vijijini, na ulipaji wa bili za huduma mbalimbali za umma kama vile maji na umeme. Asilimia 45 ya watu wa mjini na vijijini wanafanya miamala ya fedha kupitia simu za mkononi.


Serikali imeanza kutumia fursa hii kutengeneza mfumo wa Huduma za Serikali kwa Kutumia Simu za Mkononi. Mfumo unaorahisisha upatikanaji wa huduma za umma kupitia simu za mkononi kwa haraka na kwa ufanisi. Wakala imeandaa utaratibu wa kuwezesha taasisi za umma kutoa huduma kwa kutumia simu za mkononi ili ziweze kutatua matatizo ya wananchi wengi wanaotumia simu za mkononi mijini na vijijini.

Utaratibu huo ni pamoja na ugawaji wa namba za USSD kwa kutumia namba *152*00# - *152*99#. Utaratibu huu unalenga kuziunganisha taasisi mbalimbali za utoaji wa huduma kwa umma kwa kupitia simu za mkononi katika mfumo mmoja wa huduma za serikali kupitia simu za mkononi. Taasisi tano kati ya taasisi 17 zilizojisajili zinatumia mfumo huo.

# Mfumo wa Serikali wa Huduma za Ujumbe Mfupi wa Simu za Mkononi

Taasisi za Serikali zimekuwa zikitumia fedha nyingi kwa kutafuta kampuni mbalimbali zitakazoweza kuzisaidia katika kutoa huduma ya kutuma ujumbe mfupi kwa wananchi. Hii imesababisha wakala kutengeneza mfumo wa GovSms kwa lengo la kuziwezesha taasisi za Serikali kuwahudumia wananchi kwa urahisi kwa kuwatumia ujumbe mfupi wa maandishi utakaowataarifu kuhusu huduma mbalimbali zinazotolewa na Serikali.

Mfumo huu utaziwezesha taasisi za Serikali kutuma ujumbe kwa wingi "bulk sms" kwa wakati mmoja na kuboresha utoaji huduma kwa Umma, pia utaupunguzia Serikali gharama iliyokuwa ikipata hapo awali.



# Taarifa ya Fedha

Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu hesabu za mapato na matumizi ya Wakala kwa mwaka unaoishia Juni 2014

# Taarifa ya Fedha

Kwa mara ya kwanza katika historia ya Wakala, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amekagua hesabu za mapato na matumizi ya Wakala kwa mwaka unaoishia Juni 2014 na kutoa hati safi. Miaka ya nyuma, mahesabu yetu yalikuwa ni sehemu ya mahesabu ya Wizara mama.

2.0 **Audit report on the Financial Statements**

To: Chairperson Ministerial Advisory Board,
e-Government Agency (eGA),
P. O. Box 4237,
DAR ES SALAAM

RE: REPORT OF THE CONTROLLER AND AUDITOR GENERAL ON THE FINANCIAL STATEMENTS OF e-GOVERNMENT AGENCY FOR THE YEAR ENDED 30TH JUNE, 2014

**Introduction**
I have audited the Financial Statements of the e-Government Agency which comprises of the Statement of Financial Position, Statement of Comprehensive Income, Statement of Changes in owner's Equity, Statement of Cash Flows and Notes and Accounting Policies for the year ended 30th June, 2014as shown in Annexure I of this report.

**Management Responsibility for the financial statements**
The preparation of the financial statements is the responsibility of the management of the e-Government Agency as per the Statement of Management responsibility on the Financial Statements enclosed in this report as Annexure II.

Sect. 25(4) of the Public Finance Act No. 6 of 2001 (revised 2004), places responsibility on the Accounting Officer to prepare financial statements for each financial year which presents true and fair view of the financial position, financial performance and cash flows for the year then ended. It also, requires management to ensure that the reporting entity keeps proper accounting records, which will disclose with reasonable accuracy its financial position of the reporting entity and its responsibility in safeguarding the assets of the reporting entity.

**Responsibilities of the Controller and Auditor General**
My responsibility as an auditor is to express an opinion on these financial statements based on my audit. I conducted my audit in accordance with International Standards of Supreme Audit Institutions and such other procedures I considered necessary in the circumstances. These standards require that I comply with ethical requirements and plan and perform the audit to obtain reasonable assurance whether the financial statements are free from material misstatement.

An audit involves performing procedures to obtain audit evidence about the amounts and disclosures in the financial statements. The procedures selected depend on the auditor's judgment, including the assessment of the risks of material misstatement of the financial statements, whether due to fraud or error. In making those risk assessments, I considered the internal control relevant to the e-Government Agency's preparation and fair presentation of the financial statements in order to

Office of the Controller and Auditor General AR/CG/eGA/2013/2014 5

In addition, Sect. 10 (2) of the PAA No. 11 of 2008 requires me to satisfy myself that the accounts have been prepared in accordance with the appropriate accounting standards and that; reasonable precautions have been taken to safeguard the collection of revenue, receipt, custody, disposal, issue and proper use of public property, and that the law, directions and instructions applicable thereto have been duly observed and expenditures of public monies have been properly authorized.

Further, Sect 48(3) of the Public Procurement Act No.7 of 2011 and Reg. Nos. 137 (3 b) and 269 (1)of the Public Procurement Regulations2013 require me to state in my annual audit report whether or not the auditee has complied with the provisions of the Law and its Regulations.

I believe that the audit evidence I have obtained is sufficient and appropriate to provide a basis for my audit opinion.

**Unqualified opinion**
In my opinion, the financial statements present fairly, in all material respects, the financial position of the e-Government Agency as at 30thJune2014 and its financial performance and its cash flows for the year then ended in accordance with the International Financial Reporting Standards (IFRS).

**Report on Other Legal and Regulatory Requirements**
**Compliance with Procurement Legislation**
In view of my responsibility on the procurement legislation, and taking into consideration the procurement transactions I have reviewed as part of this audit. I state that the e-Government Agency has generally complied with the requirements of the PPA No.7 of 2011 and its underlying Regulations of 2013.

Prof. Mussa J Assad
CONTROLLER AND AUDITOR GENERAL

January, 2015

# Habari katika Picha



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora Mhe. Kapteni Mstaafu George Huruma Mkuchika (Mb), akiwa katika banda la maonyesho la Wakala ya Serikali Mtandao wakati wa Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika Juni 16-23, 2014 katika viwanja vya Mnazi Mmoja Jijini Dar es Salaam. Kushoto ni Mtendaji Mkuu wa Wakala Dkt. Jabiri Bakari.*

# Maonyesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma 16 – 23 Juni 2014

Wakala ya Serikali Mtandao ilishiriki maonyesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma kati ya taasisi 88 kuanzia tarehe 16 hadi 23 Juni, 2014 katika Viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam. Maonyesho hayo yalifunguliwa na rasmi na Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Utawala Bora Mhe. Kapteni Mstaafu George Huruma Mkuchika katika Viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam na kufungwa na Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi Ombeni Sefue.

Katika Maonesho hayo, Wakala ilionyesha huduma mbalimbali zinazotolewa na Wakala pamoja na machapisho mbalimbali. Zaidi ya wananchi 530 ikiwa ni wastani wa wananchi 66 kwa siku wakiwemo viongozi mbalimbali wa kitaifa walitembelea banda la Wakala na kupata ufafanuzi zaidi juu ya huduma zinazotolewa na Wakala. Wakala ilikuwa Mshindi wa tisa (9) kati ya washindi 10 katika tuzo ya Ubunifu katika utoaji wa huduma kwa umma.



*Katibu wa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, Bw. Xavery Daudi akisikiliza maelezo ya huduma za Wakala kutoka kwa Mkurugenzi wa Usimamizi wa TEHAMA wa Wakala Bw. Benedict Ndomba katika banda la Wakala wakati wa Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma Viwanja vya Mnazi Mmoja, Jijini Dar es Salaam.*




*Katibu Mkuu, Wizara ya Kazi na Ajira, Bw. Eric F. Shitindi akisikiliza jambo kutoka kwa Mtendaji Mkuu wa Wakala Dkt. Jabiri Bakari alipotembelea banda la Wakala wakati wa Wiki ya Utumishi wa Umma, katika Viwanja vya Mnazi Mmoja, Jijini Dar es Salaam. Kushoto ni Mchambuzi Mkuu wa Mifumo, Bi. Fatma Mgembe.*




*Mchambuzi wa Mifumo wa Wakala, Bw. Yakuba Yusuph akifafanua jambo .....mmoja wa wananchi waliofika katika banda la Wakala kuona huduma zitolewazo wakati wa Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma  katika Viwanja vya Mnazi Mmoja, Jijini Dar es Salaam.*



*Mchambuzi wa Mifumo wa Wakala Bw. Said Mawenje akiwaeleza wananchi waliofika katika banda la Wakala kuona huduma zinazotolewa na Wakala wakati wa Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma katika Viwanja vya Mnazi Mmoja, Jijini Dar es Salaam.*

# Mwelekeo wa Kimkakati na Hitimisho

Kwa sasa, Serikali Mtandao ni sehemu ya ajenda ya maendeleo ya Tanzania ambapo inawezesha ushiriki wa jamii katika kuwasiliana na Serikali na kurahisisha upatikanaji wa taarifa na huduma za Serikali ambavyo kwa pamoja vinaashiria utawala bora.

Kutokana na umuhimu wa TEHAMA katika maendeleo ya nchi, Wakala ya Serikali Mtandao itaendelea kuhakikisha matumizi ya TEHAMA yanaboresha shughuli za Serikali, na kuleta tija na ufanisi katika utoaji huduma kwa umma. Pia, Wakala itaendelea kujenga imani kwa watumiaji wa TEHAMA kwa kuweka mikakati yenye kurahisisha gharama na kuwezesha upatikanaji wa huduma salama zinazolingana na thamani ya fedha. Mojawapo ya mikakati hiyo ni kuhimiza matumizi shirikishi ya rasilimali zinazoendeleza jitihada za Serikali Mtandao.

Aidha, Wakala inatambua umuhimu wa TEHAMA kama kichocheo cha kuwezesha Serikali kufikia malengo iliyojipangia katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA II), Mpango wa Miaka Mitano ya Maendeleo, Mipango ya Kiuchumi na Kijamii na Vipaumbele Mahususi vya Sekta kama vile Matokeo Makubwa Sasa "BRN". Hivyo, ili kuendana na juhudi za Serikali za kutumia TEHAMA kama nyenzo za kuboresha uendeshaji wa shughuli zake, Wakala imepanga kutekeleza maeneo ya kipaumbele yafuatayo ili kuwezesha utoaji huduma bora zaidi kwa umma:-

- Kujifunza kutoka nchi zilizoendelea na zinazoendelea zenye mazingira ya kijamii, kisiasa na kiuchumi yanayofanana na Tanzania, na kutumia vigezo vya ubora vitakavyopatikana katika kuharakisha utekelezaji wa Serikali Mtandao hapa nchini.
- Kutumia fursa za serikali mtandao kuwezesha makundi ya wananchi kuwasiliana na serikali na kushiriki katika mijadala mbalimbali ya kitaifa pamoja na kutoa maoni katika kutayarisha Sera ili kuhakikisha ushiriki mkubwa wa wananchi.
- Kutoa kipaumbele cha utoaji huduma kwa wananchi kwa kutumia njia za mawasiliano za gharama nafuu zilizopo kama vile simu za mkononi.
- Kuwekeza katika kujenga uwezo wa watumishi na uelewa wa wananchi kuhusu serikali mtandao katika ngazi zote.
- Kutumia mbinu ya utekelezaji ya: "Anza na jambo rahisi na endelea na lililo tata" katika kutekeleza miradi ya Serikali Mtandao, ikiwa ni pamoja na kuanzisha miradi endelevu ya kuiletea kipato Wakala.
- Kuwezesha Serikali kuwa na miundombinu imara ya TEHAMA, stadi pamoja na vifaa kwa kutoa msaada wa ushauri na kiufundi.
- Kuboresha faharasa ya Umoja wa Mataifa "e-Government United Nations Index" kutoka tarakimu tatu hadi mbili katika tathmini itakayofuata, na kama nchi kuwa miongoni mwa nchi bora hamsini katika matumizi ya Serikali Mtandao ifikapo mwaka 2017.

## MUUNDO WA MPANGO MKAKATI WA WAKALA YA SERIKALI MTANDAO

